

# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL5

## KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS

### SEHEMU YA A (Alama 20 )

#### USHAIRI

##### 1. LAZIMA

Baba amenisomea, barua yenye thamani,  
Mama kaniandikia, kinda niliye mtini,  
Tabu haikanitoa, mama yangu simuoni,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.  
Sauti uliyotoa, imenigusa moyoni,  
Mara kuikumbukia, haingia kilioni,  
Nalia mie Radhia, mama yangu simuoni,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.  
Maneno kayasikia, hadhani uko mekoni,  
Mbio nikachungulia, nikalia sikuoni,  
Huzuni imeningia, mama nitafanya nini?  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia  
Kuku anaangalia, vitoto vyake uani,  
Kimojapo kikilia, hatulii asilani,  
Yuko radhi kujifia, chanawe kukiauni,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.  
Hata paka nakwambia, si mbwa wal si nyani  
Kamwe hawatakimbia, kuacha wana mtini,  
Lakini mie Radhia, nimetupwa majanini,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.  
Hizi tunu za dunia, zisikufanye haini,  
Wengi wanazililia, na haweshi usikini,  
Asipokupa jalia, hukupata asilani,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

Wangapi wamepumua, wenye urembo wa shani,  
Ngoma walijichezea, wakakita furahani,  
Zao zimejishia, hako wa kuwathamini,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.  
Haya yamekuchochea, uniache majanini  
Mwanao mie Radhia, nibakie ukiwani  
Mama utasimulia, kesho mbele ya manani,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.  
Kinda ninashitakia, kwa wadudi Rahamani,  
Summbukuku naumia, sasa nimo msibani,  
Mama umenikimbia, nemekosa neno gani?  
Mama yoo masikini , kinda ninakulilia.  
Nimekonda kwa kulia, ghuma haishi moyoni,  
Pengine nitajifia, kwa majonzi na huzuni,  
Usije kunililia, nizikwapo kaburini,  
Mama yoo masikini, kinda ninakulilia.

### **MASWALI**

- a) Lipe shairi mada mwafaka.
- b) Fafanua toni ya shairi hili.
- c) Nini kinachosababisha hali ya mtunzi?
- d) Huku ukitoa mifano miwili tambua mbinu za lugha zilizotumiwa katika shairi.
- e) Andika ubeti wa tisa wa lugha tutumbi (nathari)
- f) Eleza aina moja ya uhuru wa mtunzi katika shairi.
- g) Eleza maana ya msamiati huu kwa mujibu wa shairi.
- h) Ghuma
- i) Sumbukuku

## **SEHEMU YA B (Alama 20 )**

### **RIWAYA**

2.

**KIDAGAA KIMEMWOZEA: Ken Walibora.**  
**Jibu swali la 2 au la 3**

2. ...wanaume wangewastahi wanawake kidogo, wawaone kama abiria wenzao katika mashua, dunia ingekuwa pahala pema zaidi pa kuishi.

- a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
- b) Taja na ueleze sifa mbili za mzungumzaji. (alama 4)
- c) Eleza mbinu mbili za lugha ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)
- d) Onyesha jinsi wanaume wanavyokandamiza wanawake katika riwaya hii. (alama 8)

## **AU**

3. Uhuru wanaojivunia wanatomoko ni ule wa bendera tu. Thibitisha kauli hii ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea .

## **SEHEMU YA C (Alama 20 )**

### **TAMTHILIA**

#### **3. MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE**

#### **Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Safi! Safi! Huyu nitamfurusha. Hatamu mpya na mipango mipya."

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Taja mbinu zozote mbili za uandishi huku ukitolea mifano kwenye dondoo. (alama 4)
- c) Jadili uhusiano uliopo kati ya msemaji na maudhui yafuatayo: (alama 12)
  - i) Unafiki
  - ii) Propaganda
  - iii) Ubadhirifu
  - iv) Usaliti

5. Tamthilia ya Mstahiki Meya ni kiakisi cha Mataifa ya Ulimwengu wa Tatu. Jadili.

## **SEHEMU YA D (Alama 20 )**

### **DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE:**

4. 6. "Nashangaa vile kwetu tunavyoabudu watu hao wasiojali".

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Fafanua sifa za msemewa. (alama 6)
- c) Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)

## **AU**

7. Diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine imesheheni uozo wa kijamii unaolemaza nchi zinazoendelea. Jadili ukirejelea hadithi zozote tano.

## **SEHEMU YA E (Alama 20 )**

### **FASIHI SIMULIZI**

5. 8. a) Fafanua maana ya soga katika fasihi simulizi. (alama 2)
- b) Eleza sifa zozote nne za ushairi simulizi (alama 4)
- c) Maigizo ni nini? (alama 2)
- d) Eleza sifa tatu za maigizo. (alama 6)
- e) Dokeza majukumu matatu ya misimu. (alama 3)
- f) Taja sifa tatu za miviga. (alama 3)